# MUHTASALI WA KIKAO CHA KWANZA CHA VIONGOZI CHA MWAKA 2025 KUHUSU KUPANGA VIPAUMBELE VYA KANISA KILICHO FANYIKA . TAREHE 9/1/2025

**WALIO HUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mr Felix Msigala | Mwenyekiti |
| 2. | Edward Tinda | Katibu |
| 3. | Mchungaji Victor Uisso | Mchungaji |
| 4. | Alfred Luzabiko | Mjumbe |
| 5. | Wema Msigala | “ |
| 6. | Harrieth Mng’ong’o | “ |
| 7. | Happy chaula | “ |

**AJENDA ZA KIKAO**

1. KUFUNGUA KIKAO
2. KUPATA MAELEZO MAFUPI KUTOKA KWA MWENYEKITU NA WAJUMBE KUHUSU VIPAUMBELE VYA KANISA
3. KUPANGILIA VIPAUMBELE KULINGANA NA UMUHIMU WAKE.
4. MENGINEYO
5. KUAHIRISHA KIKAO

**KUFUNGUA KIKAO**

Kikao kilifunguliwa baada ya kumaliza ibada, saa 8:45 mchana.

**KUORODHESHA VIPAUMBELE**

Wajumbe waliorodhesha vipaumbele vya kanisa kwa mwaka 2025 kama ifuatavyo:

1. Kununua Vyombo vya mziki,
2. Kukusanya mchango wa nyumba,
3. Pesa ya Kujikimu ya mtumishi,
4. Pesa kwaajili ya umeme na Maji Kanisani,
5. Choo cha Kanisa.
6. Kuendeleza ujenzi wa Kanisa.

**KUPANGILIA VIPAUMBELE**

Kutokana na orodha ya vipaumbele vya Kanisa vilivyo orodheshwa hapo juu, wajumbe walijadiliana na kuamua kuwa vipaumbele hivi vikae katika mtiririko mzuri kutokana na Umuhimu wake:

1. **Pesa ya Pango**:- Wajumbe walijadiliana na kuona umuhimu wa Kupata pango kwa wakati na walijiridhisha kuwa kutokana na utaratibu wa kila wiki wa kukusanya mchango wa jengo, imekuwa ni jawabu zuri la kiutekelezaji na kwahiyo tumefanikiwa katika swala hili.
2. **Pesa ya Kujikimu ya Mtumishi**:_ Wajumbe walijadiliana na kuona kuwa kiwango anachopewa mtumishi kwaajili ya matumizi nyumbani sh. 50,000/= haitoshi, hivyo yakatolewa mapendekezo kuwa, Partners wanatakiwa waendelee na utaratibu wa kuchanga kila mwezi sh. 30,000/= na kuziingiza moja kwa moja kwenye account ya Mtumishi. Kwa kufanya hivyo kutasaidia kupunguza ugumu wa hali ya kifedha kwa Mtumishi .
3. **Pesa kwaajili ya Umeme**: Wajumbe walikubaliana kuwa mweka hazina ahakikishe kuwa ananunua umeme wa wiki nzima wa sh. 25,000/= na kumtumia mtumishi.
4. **Vyombo vya mziki**: Kulitolewa mapendekezo ya kuanzisha michango ya kila wiki, ilikuweza kufanikisha kupatikana kwa vyombo. Hivyo basi kutokana na vipaumbele hivyo vya juu kuwa vimepatiwa ufumbuwa, iliamuliwa kuwa kuanzia wiki ijayo tutatangaza kwa waumini wote na hivyo michango ya vyombo vya muziki kuweza kuanza kukusanywa.
5. **Maendeleo ya ujenzi wa Kanisa**;- Wajumbe walikubaliana kuwa kuanza kuendeleza ujenzi wa kanisa, usubiri kwanza hadi tutakapo pata vyombo vya mziki ndipo ujenzi uendelee.
6. **Kuhusu kuandaa miradi ya kanisa**: Wajumbe walijadiliana na kuamua kuwa itabidi tupange kikao kingine kitakacho husu kuandaa miradi, maana miradi itahitaji kuwe na UPEMBUZI YAKIFU (Visibility study) ya miradi husika.
7. **Choo Cha Kanisa**: Mjumbe mmoja (Felix Msigala) alisema kutokana na kusua sua kwa miochango ya kumalizia ujenzi wa choo. Yeye atahakikisha anamalizia sehemu iliyo baki, hivyo alisema hili la choo lisiwekwe kwenye vipaumbele.liondolewe

**MENGINEYO**

Mjumbe (Felix Msigala) alipendekeza kuwa vikao vya Viongozi ambavyo vilipendekezwa kufanyika mara mbili kwa mwezi, viwe vinafanyika siku ambazo siyo za Ibada ili kuwe na muda mzuri wa kujadiliana. Siku ya ibada ibaki kuwa ni siku ya kumtafakari Mungu tu, katika swala hili wajumbe walikubaliana, hiyo kila kikao kinapo karibia tutakuwa tunatangaziana kuwa sikugani kikao husika kitafanyika.

**KUAHIRISHA KIKAO.**

Kikao kila shirishwa saa 11:35 jioni.